

# Pambazuko

Toleo Namba 30

Jumatatu Machi 6-12, 2023



**KAMARI  
JANGA**

**FREE CHIPS**

**LUCKY  
FREE CHIPS  
400,000**

**Aaminike Daktari ama Balози Slaa? Uk. 5:**

**Bodaboda ni neema au balaa? Uk. 11:**

**Fanyeni kazi kama kwaya – Papa Uk. 14:**

**Katiba mpya chachu ya  
neema, uhuru**

**Uk. 4**

JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye  
namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

## Tahariri

## Endeleeni kutuunga mkono

**F**EBRUARI mwaka huu gazeti la Pambazuko lilishindwa kuwafikia wasomaji wake kutokana na sababu ambazo zilikuwa nje ya uwezo wetu.

Sababu kubwa ilikuwa ni kukwama kwa mfumo wa usambazaji ambao ulishindwa kuhimili idadi kubwa ya wasomaji ambao wamekuwa wakiongezeka kila siku.

Mfumo wetu ambao hauruhusu haki ya faragha (hasa namba za wanaopokea gazeti) ya kila mmoja kufahamika kwa wengine, ulikwama na kuzima, hivyo kulazimika kusaka njia nyingine ambayo itaruhusu msimamo wetu kubaki, huku usambazaji ukimudu idadi kubwa ya wasomaji wetu.

Ni kutokana na msimamo huo, tukaamua kusimamisha usambazaji ili kujiridhisha na mfumo mpya na imara zaidi ambao hautoi mwanya wa kuvuruga msimamo wetu wa kulinda faragha ya kila mmoja.

Pamoja sababu hiyo, pia muda huo ulitumika kuboresha baadhi ya kurasa zetu na kuutumia kujitathmini baada ya miezi sita tangu kuanza kwa Pambazuko.

Matokeo ya tathmini hiyo yanatutaka kuongeza njia nyingine zaidi ya kuwafikia wasomaji wetu, hasa wale wasiotumia WhatsApp, hivyo hivi karibuni tutawafikia wasomaji wengine kwa mfumo wa meseji za kawaida katika simu zao za mkononi.

Ingawa mfumo huo, utahitaji rasilimali fedha, tumeanza mchakato wa kuhakikisha tunapata fedha za kununua vifaa na mfumo utakaowezesha hilo kufanikiwa.

Mhariri Mkuu, kwa niaba ya bodi na watendaji wa Pambazuko na Chama cha Waandishi (Tampa) ambao ndiyo wachapaji wa gazeti hili, anaomba radhi kwa wasomaji wote kwa kutokuwa hewani.

Hakika simu, barua-pepe na mawasiliano mengine kutoka kwa wasomaji wakiuliza hatma ya Pambazuko, zimetupa nguvu ya kuhakikisha gazeti hili linaendelea kuwafikia wote kila wiki – bure bila kukosa.

Tunaamini kwamba wasomaji wetu wote wataendelea kuwa nasi na kutusoma na kusambaza gazeti kwa wengine ili Pambazuko liwe na familia kubwa zaidi inayopata habari, kuelimishwa na kuburudishwa na gazeti hili.

Pia, tunapenda kuchukua fursa hii adhimu, kwa upekee kabisa kukushukuru wewe mpenzi msomaji wetu kwa kuendelea kutuamini na hata kuwa nasi hata sasa wakati tumefika miezi sita tangu kuanza kukuletea gazeti hili.

Pambazuko limeendelea kuwa na idadi kubwa ya wasomaji wake, siyo walioko Tanzania tu, ama maeneo mengine ya Afrika, bali hata Ulaya na Marekani ambako tuna maelefu ya wasomaji wetu.

Zaidi sana tumekuwa tukipokea mapendekezo ya kutoka kwa baadhi ya wasomaji wetu wakiomba tuanze kuza Pambazuko hata kwa bei ndogo. Tunashukuru sana mawazo na matamania yao, lakini sisi tunaamini kupata habari ni haki ya binadamu – kama ulivyo mmeng'enywa wa chakula cha mwili – usivyokuwa na ubaguzi, ndiyo hata chakula cha ubongo kisibague, labda walaji wenyewe.

Hivyo, Pambazuko litandelea kumfikia kila mtu BURE.



Baadhi ya wachuuzi wa usafiri wa pikipiki (Bodaboda) wa maeneo ya Usa River, Arusha wakiwa na mabango yenye ujumbe kwa Rais Samia Suluhu Hassan wakati alipokuwa akihutubia wananchi wa eneo hilo jana. (Picha na Ikulu).

## Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: pambazuko1@protonmail.com** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

## **NUKUU**



Idadi ya watu imeongezeka Tanzania, miundombinu ya kilimo bado ni ileile ya kulima katika mfumo duni na kutegemea hali ya hewa, huku mabadiliko ya tabia nchi yakiathiri zaidi usalishaji. Kuna balaa kubwa mbele; njaa, umasikini na kuwepo kwa bei kubwa ya vyakula. Tubadilike, tuwe wabunifu – Godbless Lema, mbunge wa zamani wa Arusha.

## Tafakuri

## Katiba mpya chachu ya neema, uhuru

Na Plato HEKIMACHIUS

**M**WANGWI wa kilo cha kutaka kuwepo Katiba mpya, hatimaye ziliingia masikioni mwa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na kuamua kufanya uamuzi wa kihistoria kwa kuridhia kufufua mchakato wa kupatikana kwa Katiba mpya nchini Tanzania.

Uamuzi huo ulikuwa umezima - kwa muda, kelele za madai ya katiba mpya ambazo zimekuwa zikipazwa na Watanzania wengi, bila kujali itikadi zao; wamo wanachama wa CCM, hata kama wanadai kimyakimya na wenzao kutoka vyama shindani, hasa Chama cha Demokrasi na Maendeleo (Chadema).

Pamoja na uamuzi huo kuonyesha utayari, zipo hisia kwamba huenda umefanywa kwa nia iliyojificha kuliko dhati inayoonekana ama kusikika kutoka kwa baadhi ya viongozi wa chama hicho tawala.

Mchakato wa kupatikana kwa Katiba mpya ulianzishwa na kumalizwa na Rais Jakaya Kikwete mwenyewe, ambaye awali aliuaminisha umma kwamba kabla ya kuondoka kwake madarakani, Novemba 5, 2015, angeacha Tanzania ikiwa na Katiba mpya ambayo huenda ingekuwa na majawabu ya changamoto nyingi zinazozinga ustawi wenye neema kwa wananchi wake.

Kimsingi, uamuzi huo umeibua “tuhuma nzito dhidi ya CCM.” Kwamba watu wanahoji kiwa kweli CCM imeamua kwa dhati au imewapa watanzania “mdoli” ili wachezee na kupunguza kelele? Tuhuma hizi zisipuuzwe kwa sababu zina mashiko.

Mmoja wa kada maarufu na mjumbe wa Kamati Kuu ya CCM amesikika akisema, “tumeridhia mchakato uanze, lakini hatukusema ni lini? Yaweza kuwa baada 2025”.

Mmoja wa makamu mwenyekiti mstaafu amesema -“tumeruhusu, lakini hatukusema tuanze wapi?”



Mikono

Kauli hizi mbili zinaashiria hitaji la mjadala mpana wa ujio wa katiba mpya hapa nchini.

Kinachoonekana wazi ni hitaji la watu wapya wa kutuletea katiba mpya. Tunahitaji viongozi wapya na wananchi wapya ili waweze kutuletea Katiba mpya kupatikana.

Watu wa zamani hawawezi kutuletea katiba mpya. Baadhi ya watu wa zamani ni wale ‘waliotekwa’ na kuvuruga mchakato ule wa awali. Waliotekwa katika mchakato ule wanahitaji kufanywa wapya ili waweze kutuletea Katiba mpya.

Maswali ya msingi yanayohitaji upya wa wahusika ni tuanze lini? Tuanze wapi? Tukamilishe lini na kwa nini?

Majibu ya maswali haya yamepatikana kutoka kwa Watanzania ambao wanaamini kuna manufaa makubwa kuwa na Katiba mpya kuliko kuendelea kuweka viraka kwenye Katiba ya zamani ambayo imejaa mazingira ya chama kimoja na uimla unaopitwa kwa kasi na mazingira ya sasa.

Ni vyema basi, Katiba mpya ikapatikana mapema kuliko kusubiri wakati mwingine ambao unaweza kuleta ukakasi na kuonekana hata waliohabikia uamuzi wa CCM, waliamua “kuwapaka wananchi mafuta kwa mgongo wa chupa” kwa maslahi ya chama chao na binafsi ya viongozi wao.

## **Aaminike Daktari ama Balozi Slaa?**

**Na Luqman MALOTO**

**M**WANAFALSAFA na bingwa wa sayansi ya siasa wa Ugiriki, Aristotle, katika shairi lake la “Tragic Hero”, aliandika; shujaa lazima awe mtukufu. Baadaye shujaa atakengeuka. Kadiri atakavyobadilika utukufu hupungua na ushujaa hutoweka.

Tanzania na dunia ilimshuhudia Dkt. Willibrod Slaa, akipanda juu kabisa ya kilele cha siasa nchini Tanzania. Kila alichogusa kilionekana dhahabu. Maneno yake yaliheshimiwa utadhani Zaburi.

Hata hivyo, kwa kiasi kikubwa inaelezwa kwamba – kwa sasa Balozi Slaa haaminiki. Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), amacho alikuwa katibu mkuu wake, wanamwona ni “shujaa aliyeoporomoka”.

Aliwahi kuwa shujaa, akabeba matumaini ya harakati zao kisiasa, lakini baadaye akakengeuka. Ni shujaa ambaye sasa anaonekana kutitia kwenye tope la usaliti kwa wale waliomuamini akiwa Chadema.

Slaa alipojitoa Chadema, alikizodoa na kukipa kila aina ya ubaya na aliamini kwamba chama hicho kikuu cha siasa Tanzania hakitabaki salama. Katika kukomelea “mabaya na dhambi ya Chadema,” mwanasiasa huyo akaandika kitabu; “Nyuma ya Pazia; Chadema ilivyosalitiwa 2015.”

Kwa uthubutu mkubwa, Slaa ambaye baadaye alipewa hadhi ya kuwa balozi, alimtetea sana aliyekuwa Rais wa Tanzania, John Magufuli kuhusu shambulio la “kumiminiwa mvua ya risasi” kiongozi mwenzake ndani ya Chadema, Tundu Lissu.

Akaituhumu Chadema kuwa chama kinachoteka nyara watu. Akasema aliyekuwa Mwenyekiti wa Chadema Wilaya ya Temeke, Dar es Salaam, Joseph Yona, alitewka, akaumizwa na Chadema.

Hata hivyo, pamoja na yote hayo, Slaa wiki iliyopita aliibukia Karatu kwenye mkutano wa Chadema. Kuonekana



**Dkt. Willibrod Slaa**

akipewa jukwaa na chama hicho kumezua mgwanyiko ndani ya chama hicho, hasa vijana Chadema. Wengi wamechukizwa Balozi Slaa kupewa jukwaa kuzungumza.

Pamoja na Slaa kukisia chama hicho kwenye jukwaa hilo kwamba kimekomaa kuweza kushika dola, bado vijana wanaona hakupaswa kupewa fursa kwenye mkutano huo.

Wapo vijana wanahoji, Slaa amesahau nini Chadema baada ya kuongea yote na “kukipaka shombo” chama hicho kuwa kinatoka watu nyara?

Pia wapo wanaoona hakuna shida kwa Slaa kupewa jukwaa na wanaeleza wakisimamia msembo wa Kiswahili; “mwenda omo na tezi ruksa kurejea ngamani.”

Mitandaoni Slaa anashambuliwa. Chadema hawamwamini. Lissu na Godbless Lema, wanarejea nchini baada ya kuishi uhamishoni, wanapata mapokezi ya kishujaa. Enzi za Slaa Chadema, Lissu na Lema walikuwa wapesi mno mbele yake.

Ni hivi, Lissu na Lema bado wana “imani” kubwa Chadema. Slaa alishapoteza. Anavyopambana kuheshimiwa Chadema, anakutana na dharau, kejeli.

Slaa anaonekana kuitaka tena ushujaa, lakini ataweza ndani ya chama kipi?

**• Makala haya yamehaririwa kukidhi vigezo na hadhi ya Pambazuko**

## Uchambuzi

## Tuubane mapema ufisadi unaomea

Na Scovy MANASE

**M**ARA kadhaa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Majaliwa Kassim Majaliwa, amesikika akifoka, akionekana kukerwa na zaidi sana akithibitika kukasirika kwa matukio anayoyataja kuwa ni ubadhirifu na matumizi mabaya ya ama madaraka au fedha za walipakodi anapokuwa katika ziara za kukagua miradi ya maendeleo.

Ikumbukwe kuwa Septemba 8, mwaka jana, Majaliwa akiwa katika ziara ya kukagua miradi ya maendeleo katika Mkoa wa Tabora, alifika kwenye mradi wa ujenzi wa Chuo cha Veta Uyu, ambako alishangazwa kusikia kuwa kibanda cha mlenzi wa chuo hicho kimegharimu Sh. milioni 11.

Majaliwa alisema kwa muonekano, kibanda kile hakiwezi kuchukua kiasi hicho cha fedha alichelezwa na kwamba huenda kuna ubadhirifu umefanywa na kuamuru Taasisi ya Kuzuia na Kupambana Rushwa (Takukuru) kuwakamata na kuanza kuwachunguza wote waliohusika katika mchakato wa ujenzi huo.

Hiyo haikuwa mara ya kwanza kwa kiongozi huyo mkuu wa shughuli za serikali bungeni na mshauri -mtendaji wa karibu kabisa wa Rais Samia Suluhu Hassan, akifoka na kuamuru watendaji kukamatwa akiwa kwenye kadamnasi.

Pamoja na kwamba ni hatua nzuri kwa kiongozi wa juu kuonekana kukwera na yanayoendelea katika utekelezaji wa majukumu ya kuhakikisha maendeleo yanapatikana, bila kuwaibia wananchi kodi zao, bado kuna maeneo ambako Rais Samia, Majaliwa na uongozi mzima wa serikali, wameshindwa kuonyesha hasira zao.

Maeneo hayo ni yale yanayothibitika katika vitabu vya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwamba kuna wizi mkubwa wa fedha za walipakodi wa Tanzania na hata zile zinazoletwa kwa njia ya mikopo na hata misaada kutoka



Majaliwa Kassim Majaliwa,

nchi washirika wa maendeleo.

Kila mwaka CAG amekuwa akiibu madudu ya kutisha katika halmashauri, taasisi, wakala, kampuni na hata mashirika yanayoendeshwa na serikali moja kwa moja au kuwa na ubia, lakini hasira na sauti za kufoka hazisikiki kuwa kuu na zenye ukali kwa wahusika wanaoweza kuwekwa kwenye kundi la 'mapapa wezi.'

Pamoja na ubaya wa ubadhirifu mdogo, madhara yake yanaweza kuwa makubwa ikiwa yatajikusanya hata kufikia viwango vya ufisadi, ambao una ubaya mkubwa zaidi na kuwa na madhara yanayoumiza jamii pana zaidi.

Watanania wanapenda kuona serikali ikichukua hatua kali zaidi kwa wote wanaofisidi nchi hii, hasa hao wanaobainika kukwapua fedha za maendeleo kwa manufaa binafsi. Hawawanafanya mnyororo wa umasikini kuendelea kuwafunga wengi zaidi – na hata kupokewa na vizazi na vizazi.

Ikiwa hasira za serikali zitabaki kwa "vidagaa" tu, na mafisadi papa kuachwa, basi hata uchunguzi wa CAG na ushauri wake, hautakuwa na maana zaidi ya kujaza karatasi katika kabati za ofisi za wakubwa.

## Ugomvi wateuliwa rais jipu

Na Bollen NGETTI

**I**NAVYOONEKANA Rais Samia Suluhu Hassan amekasirika kupita maelezo. Aameamua kufanya alichokiita “mabadiliko madogo” katika serikali yake wakati Baraza la Mawaziri, makatibu wakuu, manaibu na wakubwa wengine.

Akitolea ufafanuzi sababu ya kufanya “mabadiliko madogo,” Rais Samia alisema kwa kurudia mara tatu; “silipendi hili kabisa, na iwe mwisho, sitorudia kubadili huyu huku huyu kule kwa sababu unakuta waziri na naibu wake hawaelewani, au katibu mkuu na naibu wake hawaelewani, wanagombana kwa hiyo kazi haziendi.” Samia akahitimisha kwa maneno haya; “likitokea tena, wote wawili mnaogombana nitawaondosha.”

Siku iliyofuata, magazeti ya Mwananchi na Habari Leo yalibeba habari kubwa kurasa za mbele iliyofanana; “Onyo la mwisho” kuelezea “hasira za rais” ambaye aliamua kuandaa semina elekezi Jijini Arusha ili kwenda kuwafunda viongozi hao.

Inaelezwa kuwa viongozi hao wakuu waliandaliwa semina hiyo iliyoongozwa na Katibu Mkuu Kiongozi (mstaafu), Martin Luhanzo aliyepewa jukumu, pamoja na “walimu wengine” kwenda “kuwapika” wateule hao wa Rais Samia.

Wengi wanajuiliza, hivi kwanini mawaziri na wasaidizi wao au makatibu wakuu waparurane? Wanagombania nini?

Kwanza ieleweke kwamba ugomvi wa viongozi wizarani baina na kati ya wateule wa rais haukuanza leo! Moja ya mfono ambao haukuwa na kificho ni kudorora kwa uhusiano wa kikazi kati ya Jakaya Kikwete akiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini, na katibu mkuu wake, Profesa Mark Mwandosya. Hawa inadaiwa walipishana kwenye korido za wizara kama watu wasiofahamiana kabisa.

Mmoja alijiona ni msomi wa mwisho na hivyo hawezi kuelekezwa na kada tu wa chama asiyejua menejimenti ya wizara. Lakini, mwingine alijiona kuwa ni



**Rais Samia Suluhu Hassan**

mtu muhimu sana; waziri, tena wa wizara nyeti!

Kipindi kufupi kikapita na Kikwete akateuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa, hapo wawili hao wakatenganishwa. Baadaye kidogo, Jakaya akawa Rais wa Tanzania na Profesa Mwandosya “akaonja joto ya jive” kwa kipindi kirefu.

Inaelezwa kuwa makatibu wakuu wa wizara mara nyingi hujiona kwamba wao ndio wizara na wizara ni wao. Na hii ni kwa sababu wao ndio waliobeba maduhuri ya wizara. Kwamba waziri akitaka kufanya ziara ni lazima “ampigie magoti” ili apate fedha.

Ni jambo la uhakika kwamba endapo wakuu wa mahali popote pa kazi hawaelewani, hakuna tija yoyote ya maana itakayopatikana, hivyo kuelewana ni nguzo muhimu katika kutekeleza majukumu ya kila mmoja.

Chanzo kingine cha ugomvi ni “wewe umepitia mlango upi kupata uteuzi?” Yapo baadhi ya majina ya wateule ambao inaaminika kwamba hata “wakikosea namna gani” kamwe hawawezi kufurushwa kazi kutokana na “wapi walipita” hadi kuteuliwa.

Sababu nyingine ya baadhi ya wateule wa rais ni kuwa na kiburi, hasa wale wanaobadilishwa kila mara, hata wanapokosea. Kwamba hakuna baraza la mawaziri linatajwa bila jina lake kuwemo-“tje mvua lije jua.”



## Dhana Murua

### Mmiliki halali wa taifa nani?

Na Askofu Dkt. Stephen MUNGA

**M**AMBO tunayoyaona sasa hapa Tanzania, matalan kuhusiana na kelele juu ya 'tozo' za miama ya fedha ni mfano mzuri sana juu ya hoja ya umiliki wa taifa.

Mamlaka imekaa mikononi mwa nani? Nani anafanya uamuzi juu ya maisha ya watu? Nani anamilikisha mwingine madaraka? Nani anao uwezo wa kumuondoa mwingine madarakani?

Hapa ni suala zima la uwajibikaji na uwajibishaji. Kwa upande mwingine nani anayemiliki ardhi na raslimali za taifa? Nani anayetunga sheria za kuongoza na kuratibisha uendeshaji wa nchi?

Je, sheria hizo zinatungwa kwa kulinda maslahi ya nani? Ni chombo gani kina dhamana ya kusimamia tafsiri na utekelezaji wa sheria hizo? Nani anayeteua watendaji wakuu katika mhimili unaosimamia sheria?

Majibu ya maswali kama hayo ndio huonyesha ni nani anayemiliki taifa. Mambo kama hayo lazima yatiliwe maanani katika uandishi wa katiba na sheria, kwani ndio huratibisha uwiano wa matarajio ya watu.

Ikiwa watawala ndio wanaomiliki nchi, basi katiba na sheria zitatungwa kwa namna ya kulinda nafasi za watawala hao na maslahi yao. Hapo ndipo tunasema kuwa taifa lina serikali iliyopita kiasi (maximum government).

Hali kama hiyo huminya uhuru na ushiriki wa raia katika uendeshaji wa nchi. Tena hali kama hiyo huishia kubebesha mizigo ya kodi kwa raia ili kutunza serikali na mahitaji yake. Suala zima la mvutano kati ya serikali iliyopitiliza kiasi na serikali kidogo (minimum government) vinazungukia katika mambo kama hayo.

Hapa ndipo tunaingia katika upimaji wa dhana mbili muhimu katika kujua umiliki wa taifa. Dhana hizo ni demokrasia na uwajibikaji.



Nembo ya Taifa

Tukumbuke kwamba katika kuzungumzia kipengele cha 'watu' nilishughulikia kwa kiasi suala la uwajibikaji. Uwajibikaji ni dhana muhimu katika maadili ya siasa na utumishi.

Ikiwa taifa lina watu waliotengenezwa vizuri ni wazi kwamba watu hao watatengeneza jamii ya watu waadilifu wanaowajibika ipasavyo kwa jamii.

Tulizungumza pia kwamba jamii ndio muundo wa msingi katika kuundwa kwa taifa. Kwa hiyo, taifa lenye jamii ya watu wazuri wanaowajibika, ni taifa la watu wanaowajibika kwa jamii.

Katika uwelewa huo ndipo nafasi wapewazo watu, ikiwa ni katika utawala au kitaaluma, wote huzipokea kama dhamana na kama nafasi ya kutumikia jamii na kamwe siyo haki ya awaye yeyote. Uelewa huu ndio hugeuka kuwa maadili ya jamii.

Dhana nzima ya uwajibikaji ikaapo vizuri ndipo hata utengenezaji wa miundo ya kidemokrasia huwa rahisi. Iwapo yeye walivyonyavyo watu siyo haki zao, bali ni utumishi na wanatumika kwa kuwajibika kwa jamii.





**Na Evarist Chahali**  
evarist@chahali.com

## Mezani kwa Chahali

### Samia atazame upya semina elekezi

**W**IKI iliyopita, Rais Samia Suluhu Hassan aliongoza mkutano wa faragha kwa mawaziri, manaibu waziri, makatibu wakuu, naibu makatibu wakuu pamoja na viongozi waandamizi wa serikali jijini Arusha.

Mkutano huo ulifanyika katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Arusha (AICC).

Hata hivyo, ingawa tukio hilo liliitwa mkutano wa faragha, tafsiri ya watu wengi hususan kwenye mitandao ya kijamii ilikuwa “semina elekezi”.

Semina elekezi zilifutwa na John Magfuli mara tu baada ya kuingia madarakani kuongoza Tanzania na alitanabaisha Desemba 2015 kuwa uamuzi huo uliokoa Sh. 2,000,000,000 (shilingi bilioni mbili).

Miaka minane baadaye, semina hizo zinarudishwa na yayumkinika kuwa gharama za kuendesha semina hizo zitakuwa zimeongezeka mara kadhaa.

Wakati ninatambua umuhimu wa mkutano huo wa Rais Samia na watendaji wake, ninadhani ingewezekana kupunguza gharama husika kwa njia mbadala mbili.

Ya kwanza, ni kufanyia mkutano huo jijini Dodoma ambapo hatua hiyo ingeokoa siyo tu gharama za malazi kwa watendaji wote waliokusanyika jijini Arusha, bali pia ingeepusha gharama za usafiri kwenda Arusha na kurudi kwenye vituo vyao vya kazi.

Njia nyingine ya kuepusha gharama ingeweza kuwa kufanya mkutano huko kwa njia ya mtandao. Kwamba mkutano huo ungeweza kuendesha kwa kutumia teknolojia kama ya Zoom, Microsoft Teams au Webex.

Sababu iliyonifanya nitamani kungekuwa na njia mbadala za kufanya mkutano huo ni taarifa kwamba deni la



*Rais Samia Suluhu Hassan*

taifa limeongezeka kwa shilingi trilioni 6.9 kutoka shilingi trilioni 86.5 - Januari 2022 hadi kufikia shilingi trilioni 93.4 Januari mwaka huu.

Kwa mujibu wa gazeti moja la kila siku la lugha ya Kiingereza, wataalamu wa masuala ya uchumi wameeleza kusikitishwa na ongezeko la deni hilo la taifa huku wakionya kuwa hali hiyo siyo nzuri kwa uchumi iwapo fedha zilizokopwa hazitatumika kusaidia sekta za uzalishaji mali.

Hata hivyo, serikali kupitia kwa Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini na Msemaji wa Wizara ya Fedha na Mipango, Benny Mwaipaja, alisema Watanzania hawana cha kuhofia kwa sababu fedha zilizokopwa zinaingizwa kwenye miradi ya maendeleo ambayo hatimaye italeta faida kubwa kwa Tanzania katika siku za usoni.

Lakini ni wazi, shughuli kama mkutano huo wa faragha wa watendaji wakuu serikalini ambayo yayumkinika kugharimu fedha nyingi ambazo hazisaidii sekta ya uzalishaji mali.

**Habari****Kamari janga la taifa**

Na Waandishi WETU

**W**ACHINA na matajiri kutoka Bara Ulaya na Amerika, wanawekeza mitaji yao Tanzania kuongeza ukwasi, lakini wakizidisha nguvu za maadui wa taifa; ujinga, umasikini na maradhi.

Tangu kupata uhuru wa Tanganyika, na baadaye Tanzania, Muasisi wa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alitangaza maadui hao watatu na yeye kuwa kinara wa kuwapiga vita.

Hata hivyo, miaka karibu 62 baadaye, nguvu za kuwaondosha maadui hao zinaoneka kukwama, badala yake watu kutoka nje wameruhusiwa kuja kuwapa misuli ya kuangamiza umma.

Hali hiyo inathibitishwa na uchunguzi uliofanywa na Pambazuko kwa miezi miwili kuhusu kuwepo ongezeko la uraibu wa kucheza kamari.

Pambazuko ambalo kuanzia wiki hii linaanza kuchapisha matokeo ya uchunguzi huo, limebaini vijana wadogo, wengi wakianzia miaka 12 hadi 28, wamekumbwa na uraibu wa kamari.

Vijana hao – wa kike na kiume, wamekutwa viunga vya maeneo ya Mwenge, Bunju, Msasani, Mbagala, Buza na Manzese wakicheza kamari katika baadhi ya maduka ya maeneo wanayoishi.

Pamoja na sheria nambari 4 ya michezo ya kubahatisha ya mwaka 2003 kuharamisha mashine za kamari kuwepo maeneo ya makazi ya watu, bado kuna utitiri wa mashine hizo, huku vijana hao wakicheza bila kujali muda; asubuhi, mchana, jioni na hata usiku wa manane.

Pambazuko limebaini pia wanawake, hasa wale wasiokuwa na ajira rasmi – “mama wa nyumbani,” nao idadi yao siyo haba. Katika eneo la Bunju A, Mtaa wa Chalinze pekee – wenye idadi ya kaya zinazofikia 63, kuna mashine za kamari 17 ambazo ziko kwenye maduka kinyume na sheria hiyo.

Imebainika kuwa mashine za kamari zilizoko kwenye maeneo hayo, zinamilikiwa na “wawekezaji” kutoka China, kwani ndiyo wamekuwa wakionekana – kila jioni wakipita kukusanya fedha zinazotumbukizwa na “watu masikini” kwenye mashine hizo.

Pambazuko limeeleza na mmoja wa wamiliki wa duka dogo eneo hilo, Johannes Njau, kwamba Wachina wanaomiliki mashine hizo za kamari huwalipa wenye maduka wanapoweka mashine hizo za kamari, Sh, 40,000 kila wiki.

“Hizo shilingi 40,000 ni kwa ajili ya gharama za umeme na ulinzi, hata hivyo, kuna wakati wanakunyima kama watakuta mashine haina pesa,” anaongeza Njau, kijana mwenye miaka 23.

Pambazuko ambalo limeweka kambi maeneo hayo, yanayokaliwa na watu wa kipato cha chini, limebaini kwamba kuwepo kwa mashine hizo za kamari kumeongeza uraibu, ugomvi wa familia na kwa ujumla umasikini wa familia hizo masikini.

Kwamba vijana wanaocheza kamari wamekuwa watoro shuleni na wengine kuacha kabisa “kukanyaga shuleni” wakiamini wataweza kupata “utajiri” kupitia mashine hizo za kamari.

Kijana mmoja ambaye amezungumza na Pambazuko, amekiri kwamba aliwahi kupata Sh. 10,000 baada ya kucheza Sh. 400 na kuanzia hapo “akatambua” kuwepo kwa utajiri kwenye kamari.

“Mimi niliweka Sh. 400, nikachagua simba na tembo, mara wakatokea wote na nikapata pesa nyingi, sasa kila nikipata hata Sh. 200 nakuja kujaribu bahati yangu,” anaeleza kijana huyo mkazi ya Mtaa wa Manzese ambaye ametaja jina lake kuwa ni Hamis Magela Abdallah (13).

**Habari hii inaendelea wiki ijayo.**

## Bodaboda ni neema au balaa?

**Na Dkt. Bullet RUHINDA**

**S**IKU za karibuni kumekuwapo na mjadala mkubwa sehemu mbalimbali na hasa katika makundi sogozi mitandaoni - kwamba kazi ya bodaboda ni ajira?

Mjadala huu umefuatia kauli ya mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), Godbless Lema, kwamba “kazi ya bodaboda siyo ajira, bali umasikini na umasikini ni laana!”

Kauli hii imechukuliwa kwa mitazamo tofauti huku kila upande ukitoa sababu za kukubali au kupinga kauli hiyo. Upande unaopinga unasema bodaboda ni ajira kwa sababu inahudumia watu wengi.

Kwamba kupitia bodaboda, vijana wengi wanaendesha maisha kupitia kazi hiyo kwa maana wanaweza kujenga makazi, kusomesha watoto na shughuli nyingine za kijamii, hivyo ni ajira kama zilivyo ajira nyingine.

Upande unaokataa kwamba siyo ajira, bali ni chanzo cha umasikini wanajenga hoja inayoanza kwa kuuliza maswali kadhaa mfano, “je, kuna mtu angependa mwanaye, mzazi wake au binti yake afanye kazi ya bodaboda?” Swali jingine ni kama kweli ni ajira rasmi, je kuna kodi inalipwa serikalini na waarjiriwa hao wa boda boda?

Lakini yapo maswali ya nyongeza, mfano mtu anaweza kufanya kazi ya bodaboda kwa miaka mingapi? Je, kipato kwa siku ni kiasi gani? Kinaweza kulipia bima ya afya kwa ajili ya usalama wa dereva na hata mtumiaji?

Baadhi ya watu wanadai bodaboda zimeleta umasikini zaidi kulilo ustawi kupitia ajali za kila siku ambazo zimezaa watoto yatima, wajane na walemavu.

Pia kwa vijana waliofanya kazi hiyo kwa muda mrefu sasa ni wagonjwa sugu wa kifua na mgongo, hivyo kuongeza tatizo la umasikini katika kaya kwa sababu hawana bima ya matibabu.

Je, waendesha bodaboda wanasemaje? Baadhi waliofikiwa na wanasema wanafanya kazi hii kwa sababu hawana ajira nyingine mradi tu siku ipite, lakini hawaoni mwanga mbele.

Mmoja amesema kwamba waendesha bodaboda wengi hasa mijini wanatumia boda boda za mikopo kwa maana kwamba kuna kampuni zinakopesha pikipiki kwa karibu shilingi milioni tatu kwa marejesho ya shilingi 56,000/- kila juma ndani mwaka mmoja.

Wastani wa mapato kwa siku ni kuanzia shilingi 7,000 mpaka 10,000 kwa maana kwamba baada ya marejesho muendesha bodaboda anabaki na shilingi 1,000 mpaka 3,000 kuendesha maisha na hapo bado matengenezo ya pikipiki na mafuta.

Kwa hali ya barabara zetu za vijijini na pembezi ambapo bodaboda zinatumika, ndani ya mwaka mmoja pikipiki inakuwa imechoka sana kiasi kwamba haiwezi tena kumnufaisha kijana huyo kwa muda mrefu.

Waendesha bodaboda wengine wanatumia pikipiki za matajiri ambapo wanaleta hesabu kila siku kuanzia shilingi 8,000 mpaka 10,000, na hivyo kujikuta wakati mwingine wanarejea nyumbani jioni au usiku mikonono mitupu au na kiasi kisichozidi 1,000 mpaka 3,000 ambazo hazitoshi hata kwa matumizi ya mtu mmoja achilia mbali familia.



**Bodaboda**

**Makala****Tumpe nani kulea watoto wetu?****Na Tryruckia MFINANGA**

**M**IAKA 13 iliyopita, Tanzania haikuwa na sheria ya mtoto, hivyo kila jamii, kabila na hata ukoo, ilikuwa na tafsiri yake kuhusu haki na taratibu za kuishi na kundi hilo linaloweza kutajwa kuwa ni maalum kwa kuwa lina watu wenye umri mdogo – wengi wakiwa na akili zisizokuwa pevu.

Pamoja na mtambuka huo wa haki na taratibu za kulea kundi hilo, makabila, koo na jamii zote za Tanzania zilikuwa na kazi kubwa ya kulinda maisha ya watoto, ili 'yasivurugwe' kwa maana ya kuwalinda ili nao 'wasivuruge' wanapokuwa wakubwa.

Ni kutokana na mtazamo huo, makabila, koo, na jamii nyingi – tangu enzi na enzi, zilikuwa zikiwatenga katika kazi, kula, kulala, mafunzo na hata kwenye mazungumzo rasmi ya wakubwa. Watoto walikuwa na maeneo yao maalum ya kufanya vitu vyao.

Jamii hizo za kale, zilikuwa zikiwalinda watoto na makundi ya watu wenye umri mkubwa na zaidi sana ikiwapa elimu ya kuepukana na makundi ya vijana wasiokuwa na maadili, wazembe wa kazi za nyumbani na shamba na wavuta bangi.

Kuja kwa Sheria ya Mtoto Na. 21 ya mwaka 2009 ilikuwa ni kutimiliza yale yaliyokuwa yakifanywa na jamii hizo za kale na kwa kuzingatia mazingira ya Tanzania na mikataba mingine ya kimataifa. Kamwe sheria hiyo haikuwa na jambo geni, isipokuwa tu kutaja umri wa mtoto kwamba ni yule mwenye miaka chini ya 18.

Sheria hii ambayo pia imechota maeneo kadhaa kwenye sera ya taifa ya watoto, inaweka bayana muundo unaolenga kumpa mtoto kinga pamoja na viwango kwa ajili ya utoaji haki kwa watoto, na pia kuweka misingi ya kulindwa dhidi ya maonevu yoyote na kwa namna yoyote ile.

Kwamba kila mtu ana haki na wajibu wa kulinda haki za mtoto na kudhibiti kila

**Watoto**

kinachoonekana kuingilia uhuru wake ili kumjengea mazingira bora ya kuwa Mtanzania mwema na kuwajibika kwa ajili yake, familia na hata maendeleo ya taifa.

Ni dhahiri kwamba malezi wanayopewa watoto ndiyo msingi wa mustakabali wao. Maisha ya mtu hutegemea sana msingi wa malezi aliyopata tangu angali mtoto.

Hata hivyo, pamoja na kuwepo kwa sheria hiyo, bado jamii ya sasa imegeuka kuwa katili mno dhidi ya maisha ya watoto. Idadi ambayo haifahamiki kirahisi – waliokuwa watoto wakati sheria hiyo inatungwa, wamekuwa vijana watukutu wakiwamo vibaka, wezi, majambazi, watumia dawa za kulevya na wenye kufanya biashara ya kuuza miili yao kwa ngono.

Kimsingi, mtoto hazaliwi akiwa na tabia mbaya. Hufunzwa na jamii inayomzunguka kwa njia mbalimbali. Wapo wanaopata tabia hizo ndani ya familia kutoka kwa wakubwa zao, kutoka shuleni, kutoka kwenye nyumba za ibada na kwa majirani.

Swali la kujiuliza, je, nani tumwamini kulea watoto ikiwa hata wazazi wanashiriki kuharibu mustakabali wa watoto wao.

Nani sasa?

## Uraia Pacha dhidi ya Hadhi Maalum

**S**ERIKALI ya Tanzania iko mbioni kutunga sheria itakayowawezesha wanadiaspora kupewa Hadhi Maalum inayoelezwa italinda asili ya uzawa wao.

Hata hivyo, nia hiyo ya serikali imekuwa ikielezwa na wale wenye kutaka kuwepo kwa uraia pacha, kuwa ina ukakasi, na kwamba itaendelea kuchelewesha kuwepo kwa mchango mkubwa wa Watanzania wanaoishi nje kwa nchi yao ya asili.

Jedwari hili linabeba mtazamo wa wanaoshabikia uraia pacha dhidi ya hadi maalum.

Pambazuko limeamua kutumia jedwari hili ili kuibua mjadala wa kitaifa ambao utawezesha ngazi za mamlaka kufanya uamuzi wenye mwelekeo chanya zaidi.

Endapo msomaji wetu una maoni na ushauri kuhusu jambo hili, tafadhali tuandikie kupitia email: [info@pambazuko.tz](mailto:info@pambazuko.tz) nasi tutachapisha bure.

URAJA PACHA	VS	HADHI MAALUM
Hauhitaji Mabadiliko Ya Katiba		Inahitaji Mabadiliko ya Katiba
Hauona gharama kubwa. Unochahitaji ni kubadilisha Sheria ya Uraia ya Mwaka 1995		Ni GHARAMA KUBWA kwa sababu nahitaji mabadiliko ya sheria nyingi; Uhamiaji, Andhi, Uwekezaji nk.
Tayari Katiba inatambua uwepo wa Uraia Pacha, (Ibora 5(2)a na 6(2)a).		Katiba inakatoza Hadhi Maalum kwa raia.
Unaongeza ulinzi na usalama. Katiba inamtaka raia kuwa na wajibu wa ulinzi kwa nchi.		Inaondoa wajibu wa Kikatiba wa raia kuhusu ulinzi na usalama
Unaongeza maradufu imani ya uwekezaji.		Hadhi Maalum inaweza kufutwa wakati wowote, Imani ya uwekezaji hatao.
Unalinda Utaifa, Uraia na Haki ya Kuzaliwa (birthright)		Haiongezi wala kulindo utafa, uraia na Haki ya Kuzaliwa (birthright)

## Makala

## Fanyeni kazi kama kwaya – Papa

Na Benedict MSOFE,  
Vatican

**F**EBRUARI 25, mwaka huu - 2023, katika Ukumbi wa Papa Paulo wa 6, Vatican, Papa Fransisco alipokea kundi la watu takribani 3000 wakiwemo magombera, wahadhiri, wanafunzi na wafanyakazi wa vyuo vikuu vya Kikatoliki wanaoishi na kusoma Jiji la Roma, Vatican.

Katika kusanyiko hilo, kiongozi huyo mkuu wa Kanisa Katoliki Duniani, pamoja na mengine aliyozungumza na kundi hilo, ujumbe wake mkubwa unaweza kufupishwa katika hoja moja; “fanyeni kazi kama kwaya”;

Akitumia maneno ya Askofu na Shahidi wa Zamani wa Katoliki Mt. Inyasi wa Antiokia, Papa alisema kuwa vyuo vikuu (na pia kila taasisi) vinapaswa kufanya kazi kwa kushirikiana kama kwaya.

“Imbeni kama kwaya,” ni maneno ya Mt. Inyasi. Hii ni kwa sababu ya utajiri mkubwa vinavyoubeba vyuo hivi unaodhihirishwa katika tafiti, midahalo, upambanuzi wa alama za nyakati na katika kusikiliza hekima za tamaduni mbalimbali.

Papa alisema kuwa chuo ni shule ya maelewano na makubaliano, kamwe siyo eneo la kuigana na kufanana katika yote. Hii ndiyo siri ya kwaya kuimba vizuri; yaani, maelewano na upatanifu wa sauti na vyombo.

Zipo sauti na vyombo tofauti ambavyo katika utofauti wao vinapaswa kwa pamoja visikike na kuleta uzuri unaotakiwa. Hata hivyo, Papa alisisitiza kuwa maelewano na upatanifu huu utakaonekana katika utendaji wa kwaya, ni lazima kwanza ufanye kazi ndani mwa mtu binafsi.

“Ni lazima upatanifu huu uanzie ndani mwenu, kati ya nguvu zenu tatu; nguvu ya akili, nguvu ya moyo na nguvu ya mikono,” alisema na kuongeza kwamba “tusiridhike mara zote na suluhu za muda



Papa Fransisco

mfupi pekee wala tusiitazame safari ya ukuaji kuwa ni kulialia na kujitetea tu. Na akaongeza kwamba uhalisia ni muhimu zaidi ya fikra pekee.

Akitumia mfano wa ‘Sanaa ya Yesu Mfufuka’ iliyokuwa nyuma yake, Papa alisema; “angalieni sanaa hii iliyochongwa na Pericle Fazzini. Mikono ya Yesu ni kama ya mtiribu (kwaya masta) - mkono wa kuume upo wazi kama unaongoza kwaya nzima kwa pamoja umeinuliwa kama kuashiria waimbaji katika umoja wao waongeze sauti polepole, kisha mkono wa kushoto - kidole chake kimoja kimenyooshwa kama vile kumuashiria mwimbaji mmoja binafsi kwamba ni zamu yako sasa!

Papa akaongeza katika kuitafsiri sanaa ile kwa kueleza kuwa Yesu ndiye anayeongoza na anapowaongoza wote pamoja, anamuongoza pia muimbaji mmoja.

Umoja wa kwaya nzima ni wa lazima pia, ingawa hauwezi kushinda wa kwaya nzima na Papa akaendelea kuisitiriza kuwa ni muhimu kwa kila mtu kujifunza kutumia vizuri uwezo wa mikono katika kuumba.

# **Pambazuko**

**SASA  
TUNAPOKEA  
MATANGAZO**

**EWE  
MFANYABIASHARA  
NA MTOA HUDUMA,  
ENDAPO UNAHITAJI  
KUWAFIKIA WATEJA  
WENGI ZAIDI BILA  
KUJALI MIPAKA YA ENEO  
ULILOPO, TANGAZA  
NASI KWA**

Kuwasiliana kupitia: 0744 768 263  
au Barua- Pepe; [info@pambazuko.tz](mailto:info@pambazuko.tz)



## Makala

Na Revocatus KUULI

**N**IMEFARIJKA kwa uamuzi wa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuonyesha dhamira yake kupanua, kuimarisha na kuhakikisha demokrasia inakua.

Nia ya Rais Samia kuona wananchi wake wanapata fursa ya kufurahia matakwa ya kikatiba na sheria yameleta furaha kwa wengi na siyo wanasiasa tu, bali umma wa Watanzania.

Mtazamo wa Rais Samia kwamba upo umuhimu wa kuzifanya marekebisho baadhi ya sheria zinazohusika na siasa ikiwa ni pamoja na Sheria ya Uchaguzi Ibara ya 343, unaleta faraja zaidi na kuweka nia yake njema kwenye mizani ya "mzalendo wa kweli."

Sheria zetu ya uchaguzi zimekuwa zikilalamikiwa sana na wadau mbalimbali



Rais Samia Suluhu Hassan

# Mabadiliko ya Katiba kumbeba Samia

wa siasa kuwa zinaminy demokrasia nchini, lakini pia sheria hizo zinazonekana kukiuka baadhi ya vifungu katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mambo yanayolalamikiwa ni pamoja na matokeo ya uchaguzi wa rais kutopingwa mahakama, hivyo kupingana na haki ya mtu kudai haki yake mahakamani pale mtu huyo anapoamini uchaguzi huo haukuwa huru na haki, hivyo kuhitaji msaaada wa mahakama kupata haki hiyo.

Haki ya mtu kuchagua na kuchaguliwa ni suala linalotia ukakasi katika sheria, wakati kupiga kura au kupigiwa kura ni haki ya msingi katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sheria ya Uchaguzi inaweka masharti kwa mgombea kuwa mwanachama wa chama cha siasa ili kupata sifa za kuchaguliwa huku ikitoa nafasi ya kupiga kura au kuchagua kwa kila Mtanzania mwenye umri unaoruhusiwa – miaka 18 na kuendelea.

Haileti mantiki kumpa mtu haki ya

kuchagua bila kujali uanachama wake kwa chama chochote, lakini sheria hiyohiyo ikaona mantiki ya ulazima wa mtu anayechaguliwa kuwa mwanachama wa chama fulani na hivyo kuwanyima wanachi wasiokuwa wanachama wa vyama vya siasa haki yao ya msingi ya kuchaguliwa (kupigiwa kura).

Inasikitisha zaidi kuwa licha ya mahakama kutoa uamuzi unaoruhusu mgombea binafi katika kesi maarufu ya Mchungaji Christopher Mtikila dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, bado haki hiyo imeendelea kukataliwa kama siyo kupuuzwa.

Kuna suala la mgombea wa kiti cha urais kutangazwa mshindi Kwa wingi wa jumla wa kura (simple majority), kwa namna sheria ilivyo sasa ni rahisi kumpata rais aliyekataliwa na watu wengi kuliko waliomchagua kwa mfano rais akapata asilimia 30 huku asilimia sabini zikichukuliwa na wagombea urais

# Mabadiliko ya Katiba

wengine.

Inawezekana wagombea hao wengine wamepata asilimia kubwa zikiwekwa pamoja, lakini kila mgombea kati yao hakufikisha asilimia 30 za mshindi.

Hivyo ni vyema kuwepo haja ya kumpata mshindi wa urais kwa asilimia zaidi ya 50 kwa kubadili Katiba na sheria ili mshindi wa kiti cha urais apatikane zwa zaidi ya asilimia 50 ya kura zote.

Na ili kuondokana na kanuni ya mshindi kwa kura za jumla (simple majority rule) ni muhimu Katiba na Sheria ya Uchaguzi zikaruhusu vyama kushirikiana kupata ushindi kwa kuruhusu vyama vya siasa kuungana kwa lengo la kupata ushindi katika uchaguzi (political parties coalition) au kuruhusu vyama kushirikiana kuunda serikali (Coalition Government), hali hii itasaidia kuimarisha demokrasia, kukaribisha ushirika wa kisiasa baina ya vyama vya siasa.

Kubwa zaidi ni muundo wa Tume ya Uchaguzi ambao kwa hakika unaleta ukakasi katika kusimamia na kutoa haki kwa wagombea wa vyama vyote.

Kwamba tume hiyo kuwa na makamishna wake wanaoteuliwa na mmoja wa wagombea au chama chake, kunaonekana wazi kuwepo kwa mwanya wa kutotenda haki.

Hivi kwanini wasiwepo makamisha na watendaji wengine wa tume hiyo ambao wanaajiriwa – baada ya kupitishwa kwenye mchakato mkali na wenye uwazi katika usaili; kuanzia makamishna hadi maofisa wake wengine hadi ngazi ya kata au kijiji.

Pia tume kuendelea kuwatumia maofisa wa serikali, wakurugenzi wa halmashauri kuwa wasimamizi wa uchaguzi kwenye maeneo yao, siyo sahihi kabisa.

Wakurugenzi wa halmashauri ni wajaajiriwa wa serikali ambayo inasimamia utekelezaji wa ilani na matakwa mengine

ya chama kinachokuwa madarakani, sasa kuna nafasi finyu zaidi ya watendaji hao kutenda haki dhidi ya vyama vingine vinavyowania kuingia madarakani wakati yeye akitakiwa kusimamia haki na kutenda kwa usawa.

Halafu suala la mbunge anapohama chama wakati akiwa anatumikia nafasi hiyo, kwamba anapoteza nafasi yake, halijakaa sawa na linavunja Katiba kwa kuwa huyu ni mwakilishi wa wananchi na kamwe siyo chama, kwenye chama “amepitia” tu kwa mujibu wa Katiba.

Hivyo, ni vyema mbunge anapohama chama asipoteze ubunge na hata anapofukuzwa, abaki na dhamana hiyo kwa kuwakilisha waliomchagua. Sheria ya sasa inamfanya mbunge aliyechaguliwa kuwa mwoga kwa chama chake na siyo kwa waliomtuma kwenda kuwawakilisha.

Na pia kuwepo uwezekano wa mbunge “kuwajibishwa” na waliompigia kura wakati wovote na isiwe kusubiri miaka mitano ndipo aondolewe kwa kura.

Mbadiliko haya yakifanyika, upo uwezekano mkubwa kwa Tanzania kuwa kinara wa demokrasia na utawala bora Afrika – huku wananchi wake wakipata fursa ya kufurahia matunda ya kuheshimiwa na viongozi walioko madarakani.

Pamoja na yote haya, ni vyema zaidi kukawepo sheria moja muhimu ya masuala ya uchaguzi kwa kuziungansha Sheria ya Uchaguzi ya Taifa - aya ya 343 na ile ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa - aya ya 292.

Inawezekana Rais Samia akawa ndiye “kinara” aliyekuwa akisubiriwa kuibadili nchi na kuwa na Tanzania yenye kila aina ya heri na faraja kwa wananchi wake.

Kuuli ni wakili ICC, IRMCT, AfCHPR, Mahakama Kuu Tanzania, Mahakama Kuu Zanzibar, Mkurugenzi wa Halmashauri (mstaafu) na Msimamizi wa Uchaguzi. Sasa ni Wakili wa Serikali Mkuu-Wizara ya Katiba na Sheria.

**Makala****Maadili na ustawi wa binadamu**

Na Darius RUTAZANA

**W**APO watu wachache watapinga tamko lifuatalo; “kwamba, kwa ajili ya kuhami uzima wa kiumbehai aitwaye binadamu na kukuza ustawi wake, tunapaswa kuheshimu kanuni kuhusu uzima na ustawi wa watu wote duniani.”

Lakini, kuna changamoto moja kuhusu tamko hilo; kwamba sheria za nchi moja hadi nyingine hutofautiana katika kutekeleza kanuni hizo.

Mfano, ukifananisha sheria ya kuzuia na kupambana na makosa ya jinai nchini Tanzania na nchini Kenya, utaona kwamba zinatofautiana kulingana na matakwa ya nchi husika.

Wakati sheria za Tanzania zinakataza kulima, kuuza na kuvuta mirungi, sheria za Kenya zinaruhusu. Kuna tofauti nyingi kama hizi, japo Wakenya na Wataanzania ni wanadamu wenye hulka moja.

Na kwa sababu ya hulka yao, maisha yao huongozwa na “kanuni za kibinadamu kuhusu uzima na ustawi wa watu” zilizo sawa. Mfano, wote wanavuta hewa ya oksijeni na kupumia hewa ya ukaa.

Kwa hiyo, tangu karne nyingi, wanazuoni wamekuwa na shauku ya kusanifu mfumo wa kanuni za kuratibu ustawi wa watu kwa kuzingatia ukweli huu.

Wote wanakubaliana kwamba, “kwa ajili ya kuhami uzima wa kiumbehai aitwaye binadamu na kukuza ustawi wake, kila mtu anapaswa kuheshimu kanuni za kibinadamu kuhusu uzima na ustawi wa watu.”

Lakini, wanazuoni hutofautiana pale

swali lifuatalo linapoulizwa; “kanuni hii inapaswa kutumika kila mahali, kila wakati, na kwa kila mhusika, bila kutofautisha mazingira husika?”

Kwa ufupi, kuhusu mipaka inayopaswa kuwekwa ili kubainisha ukomo wa heshima inayotajwa kuna kambi kuu mbili za kimawazo hadi sasa.

Kambi moja inatetea “nadharia kongwe kuhusu kanuni asilia za ustawi wa watu,” yaani “the old natural law (onala) theory,” au inaweza kuelezwa kuwa ni; “nadharia ya Onala.”

Na kambi nyingine unatetea “nadharia mamboleo kuhusu kanuni asilia za ustawi wa watu,” yaani “the new natural law (Nenala) theory,” au “nadharia ya Nenala.”


Je, kati ya hii mifumo miwili ya kimaadili, ni mfumo gani unapaswa kutumika ili kukuza na kuhami ustawi wa watu wa Tanzania?

Fuatilia jawabu katika makala zijazo. Lengo ni kubuni na kupendekeza nadharia ya Kiafrika kuhusu kanuni asilia za ustawi wa watu. Tunaongelea “the consolidated natural law (conala) theory,” au hapa tuseme “nadharia ya Conala.”

Kuhusu mada hizi, katika toleo la sasa, kuna taarifa za kitafiti zifuatazo; Mtafiti Ada Lovelace ametafiti na kundika juu ya “binadamu ni kiumbehai jamii ya wanyama.”

Mtafiti mwingine, Renatus Cartesius ametafiti na kuandika juu ya “kanuni za uzima na ustawi wa watu.” Na mtafiti Digna Desirata ametafiti na kuandika juu ya “jukumu la kuheshimu ustawi wa watu.”

Huu ni mfulululizo wa makala tatu zinazotegemeana katika maudhui zilizoko katika kurasa zinazofuata na zitahitimishwa katika toleo lijalo kwa kuchapisha makala nyingine.



# Binadamu na uasilia wa wanyama

Na Ada LOVELACE

**K**ANUNI asilia za kibinadamu kuhusu kuzima na ustawi wa watu, hutusaidia kujibu swali lifuatalo; ustawi wa binadamu ni kitu gani, tunamtambuaje binadamu aliyestawi, na mfumo gani wa kimaadili unapaswa kutumika ili kukuza na kuhami ustawi wa watu wa Tanzania?"

Swali hapo juu haliwezi kujibika hadi kwanza tukubaliane kuhusu "hulka ya binadamu," yaani "asili ya binadamu," yenye kutueleza "binadamu ni kiumbehai mwenye uwezo wa kufanya nini, kuwa nani, na anayo mahitaji gani."

Napendekeza kujibu swali hili kwa kutumia mawazo ya wanazuoni kadhaa. Kuna Eric Olson (2003) na makala yake, "An Argument for Animalism"; Joan Strassmann na David Queller (2009, 2010) na makala zao, "Beyond society (2009)" na "The social organism (2010)"; na Alexander Pruss (2012) na kitabu chake, "One body."


Mawazo ya wanazuoni hawa yanaonyesha kwamba binadamu ni kiumbehai mwenye sifa za kimwili kama walivyo wanyama wengine.

Hivyo, kuna kanuni asilia za kibinadamu kuhusu uzima na ustawi wa watu zinazoongoza utendaji wa mfumo mbalimbali ya kimwili. Bila kuzielewa kanuni hizi hatuwezi kuongea kwa ufanisi kuhusu ustawi wa watu.

Lakini, urazini wa binadamu ndiyo sifa pekee inayotomfautisha na wanyama baki. Urazini ni uwezo wa kufikiri, kuamua na kufanya matendo huru ya kimwili.

Hivyo, kuna kanuni asilia za kibinadamu kuhusu uzima na ustawi wa watu zinazoongoza utendaji wa mfumo wa kiakili, mfumo wa uamuzi na mifumo ya kimwili inayoratibiwa na mfumo wa akili. Pia, bila kuzielewa kanuni hizi hatuwezi kuongea kwa ufanisi kuhusu ustawi wa watu.

Wanazuoni niliowataja hapo juu, wanazigawanya sifa za viumbehai wote, na binadamu akiwemo, katika makundi makuu mawili. Kuna sifa zinazopatikana katika miili ya viumbehai wote na sifa



zinazopatikana katika miili ya baadhi ya viumbehai.

Tuanze na sifa zinazowahusu viumbehai wote. Kusudi kitu kiitwe kiumbehai, kuna sifa moja tu ya lazima, nayo ni "organismality." Napendekeza kunyumbulisha neno hili kusudi lisomeke "uoganizimalia." Wanachosema wanazuoni ni kwamba, "uoganizimalia" wa kiumbehai ni sifa inayomaanisha ukweli ufuatao;

Kwamba, kila kiumbehai ni kitu chenye sehemu nyingi zenye miundo tofauti, na zenye majukumu tofauti yanayokamilishana, yakionyesha ushirikiano mkubwa sana, na upinzani mdogo sana, katika namna ambayo inafanikisha lengo kuu moja; yaani, kulinda maisha ya kiumbehai na ukoo wake.

## Makala

## Binadamu na uasilia wa wanyama

Kwa mfano, tumbo hupokea na kusaga chakula. Mapafu huchota hewa ya oksijeni kutoka angani na kuipenyeza katika mishipa ya damu. Moyo husukuma damu ili isambaze chakula na hewa hiyo kwenye seli mbalimbali za mwili.

Seli huunguza chakula na kuzalisha nishati kwa ajili ya kuendesha shuguli za kimwili, na hivyo kulinda maisha ya mwili wote. Hatimaye, figo na vinyweleo huchuja na kutoa uchafu mwilini kwa njia ya mkojo na jasho.

Hapa tunaona viungo tofauti vya mwili vikishirikiana katika kufanya lengo la kulinda na kuendeleza maisha ya mwili, kila kiungo kikiwa na muundo wake na jukumu lake maalum.

Ushirikiano wa viungo vya mwili wenye kufanikisha lengo la kulinda maisha ya kiumbehai na ukoo wake huitwa “uoganizimalia.”

Hivyo, kuhusu “uoganizimalia” wa kiumbehai Strassmann na Queller (2009:3144) wanasema kwamba: “kiumbehai hasa ni mfumo wenye kuonyesha ushirikiano mkubwa na ukinzani mdogo katika sehemu zake za ndani.”

Kwa kutumia kigezo hiki, wanatuhimiza kufikiri nje ya sanduku la mawazo ya kimapokeo kuhusu “picha” ya kiumbehai wa kila siku, mwenye mwili uliofungashwa ndani ya ngozi au ndani ya gome.

Nje ya sanduku hili la kimapokeo, Strassmann na Queller (2010:610) wanasema kuwa, fasili yao inaonyesha kwamba, katika kila kundi lifuatalo, kuna “uoganizimalia” unaolipa sifa ya kuitwa “kiumbehai kabambe” –mfano hapa timu ya mpira wa miguu, wabunge, baraza la mawaziri, kundi la mchwa, kundi la nyuki, jozi ya ua na nyuki anayelichavusha, na jozi ya mke na mume.

Hivyo, wanatofautisha kati ya kiumbe hai mwenye mwili mmoja uliofungashwa ndani ya ngozi moja, kama vile ng’ombe na kiumbehai wa kijamii, kama vile timu ya mpira, yenye kuundwa na miili tofauti inayofungamanishwa pamoja na mpaka wa kimantiki pekee, kiasi kwamba huwezi kuona kwa macho mpaka bayana

unaozitenganisha timu mbili tofauti zinapokuwa uwanjani zinacheza mpira.

Naye, Pruss (2012:102), anaungana nao kwa kusema kwamba, “muungano wa viungo katika mwili wa kiumbehai unahusisha “uoganizimalia” wenye sifa kuu mbili, yaani kushirikiana kwa kufanya kazi tofauti zinazokamilishana katika safari ya kufukuzia lengo la pamoja,” yaani kulinda maisha ya kiumbehai na ukoo wake.

Sasa tuongeele sifa zinazowahusu viumbehai wachache. Mbali na sifa kuu ya “uoganizimalia” wa kila kiumbehai, kuna sifa za ziada, ambazo zinawahusu baadhi ya viumbehai. Tumezisoma katika vitabu vya bayolojia tangu darasa la kwanza.

Tulipokuwa sekondari mwalimu wangu wa bayolojia alinifundisha kuzikumbuka baadhi ya sifa husika kwa msaada wa maneno “MR. GREYDS.” Yaani, “movement, reproduction, growth, respiration, excretion, nutrition, death and sensitivity.”

Ndio kusema, sifa ya “kujongea kwa kusogeza mwili kutoka eneo moja hadi jingine, kuzaa mtoto, kukua kimwili, kupumua, kutoa uchafu mwilini, kula chakula, kufa, na kusoma mabadiliko ya kimazingira na kujipanga ipasavyo.”

Hata hivyo, tabia ya “kuzaa” haiwahusu viumbehai wote, maana, kuna wagumba, waseja, na matowashi, na wote hawa ni viumbehai.

Pia, kufa siyo sifa ya viumbehai wote, maana kuna viumbehai ambao sayansi inaamini hawafi. Mfano, mdudu aitwae “amiba” huwa hafi. Badala yake huzaa kwa kujigawanya mara mbili, na watoto wake wanafuata mtindo huo hadi milele ijayo.

Kwa hiyo, “kuzaa mtoto” na “kufa” ni mifano mizuri kueleza dhana kwamba kuna sifa za viumbehai ambazo ni kwa ajili ya kuvitambulisha baadhi ya viumbehai, lakini haziwahusu viumbehai baki.

Kwa ujumla, sifa za viumbe hai zilizotajwa zinaweza, na zinapaswa, kuwa msingi bora wa kubuni kanuni za maadili asilia kwa ajili ya kuhami uzima wa binadamu na ustawi wake.

# Kanuni za uzima na ustawi wa watu

Na Renatus CARTESIUS

**T**AYARI tumeona kwamba, sifa za viumbe hai zinaweza kuwa msingi bora wa kubuni kanuni za kimaadili kwa ajili kuhami uzima wa binadamu na ustawi wake.

Kwa kuzingatia ukweli huu sasa kuna uhuru wa kuongelea aina tofauti za “kanuni asilia za kibinadamu kuhusu uzima na ustawi wa watu.”

Kuna kutumia sifa za binadamu kama kiumbeghai mwenye sifa zilizotajwa katika makala zilizotangulia, kuna “kanuni asilia za kibinadamu kuhusu uzima na ustawi wa watu” zinafuata kimantiki.

Kuna kanuni ya muungano wenye sura ya sababu na matokeo ya lazima kati ya kitendo cha “kusoma mabadiliko ya kimazingira na kujipanga ipasavyo” na kitendo cha “kujongea kwa kusogeza mwili kutoka eneo moja hadi jingine,” kiasi kwamba, bila kitendo cha kwanza kitendo cha pili haliwezekani.

Kuna kanuni ya muungano wenye sura ya sababu na matokeo ya lazima kati ya kitendo cha “kupumua” kwa kuvuta hewa ya oksijeni na tukio la “kukua kimwili,” kiasi kwamba, bila kitendo cha kwanza tukio la pili haliwezekani.

Kuna kanuni ya muungano wenye sura ya sababu na matokeo ya lazima kati ya kitendo cha “kula chakula” na tukio la “kukua kimwili,” kiasi kwamba, bila kitendo cha kwanza tukio la pili haliwezekani. Badala yake kutatokea “udumavu wa kimwili.”

Kuna kanuni ya muungano wenye sura ya sababu na matokeo ya lazima kati ya kitendo cha “kula chakula” na tukio la “kutoa uchafu mwilini,” kiasi kwamba, bila kitendo cha kwanza tukio la pili haliwezekani.

Kuna kanuni ya muungano wenye



*Prof. Saul Kripke*

sura ya sababu na matokeo ya lazima kati ya kitendo cha mama “kula chakula” na tukio la “kutengenezwa kwa maziwa ya mtoto kwenye matiti yake,” kiasi kwamba, bila kitendo cha kwanza tukio la pili haliwezekani. Badala yake kutatokea “unyafuzi” au “kifo” cha mtoto anayenyonyeshwa.

Na kuna kanuni ya muungano wenye sura ya sababu na matokeo ya lazima kati ya kitendo cha “kula chakula” na tukio la “kubaki na uhai wa kimwili,” kiasi kwamba, bila kitendo cha kwanza tukio la pili haliwezekani. Badala yake kutatokea “kifo.”

Zote hizi ni kanuni zinazotaja muungano wenye sura ya sababu na matokeo ya lazima kati ya kazi mbili, moja ikiwa chanzo kinachozalisha hatima fulani, ambapo hatima hiyo ni chanzo cha hatima inayofuata katika mnyororo mrefu wa sababu na matokeo ndani ya mwili.

Kwa kuhitimisha basi, tunaweza kusema yafuatayo; fikiria kwamba, kuna kazi mbili zilizotehwa sehemu ya kanuni moja ya kibinadamu kuhusu uzima na ustawi wa watu, ambapo kazi ya kwanza ni sababu na kazi ya pili ni matokeo yake.

## Makala

## Kanuni za uzima na ustawi wa watu

Inatoka Uk. 21

Basi, kwa sababu hii, kazi ya kwanza isipofanyika kazi ya pili haitafanyika pia.

Hii maana yake ni kwamba, bila kujali kama ni kwa mpito au kwa utaratibu wa kudumu, kwa kiasi fulani au kwa ujumla, jaribio lolote la kuzitenganisha kazi hizi mbili za kimwili zinazotegemeana katika mtindo wa sababu na matokeo, linaweza kuhujumu uzima na ustawi wa kiumbehai hicho, ama kwa mpito au kwa utaratibu wa kudumu, ama kwa kiasi fulani au kwa ujumla.

Tunaweza kuelewa na kukubali tamko hili kama mambo matatu yafuatayo yatabainishwa vizuri, kama ninavyofanya hapa chini.

Mosi, kila kanuni ya kibinadamu kuhusu uzima na ustawi wa watu iliyotajwa hapo juu, inahimiza “utaratibu wa kuheshimu sababu pamoja na matokeo yake kwa mpigo,” yaani “both/and scenario.”

Utaratibu huu unahimizwa kwa kuwa, pasipo kufanyika kwa kazi ya kwanza, ambayo ni sababu, kazi ya pili ambayo ni matokeo haifanyiki.

Pili, kila kanuni ya kibinadamu kuhusu uzima na ustawi wa watu iliyotajwa hapo juu, inaukataa “utaratibu wa kuheshimu sababu na kudhuru matokeo yake au kuheshimu matokeo na kudhuru sababu yake.

Utaratibu huu unakataliwa kwa kuwa, pasipo kufanyika kwa kazi ya kwanza, ambayo ni sababu, kazi ya pili, ambayo ni matokeo,

haifanyiki; na vivyo hivyo kazi baki zinazotegemea kufanyika kwa kazi ya pili hazitafanyika.

Hivyo, kazi ya pili isipofanyika kwa sababu ya uamuzi wetu, tunakuwa tumesababisha kwa makusudi utengano katika muungano uliopo kati ya sababu na matokeo yake ya lazima, bila kujali kama ni kwa mpito au kwa utaratibu wa kudumu, kwa kiasi fulani au kwa ujumla.

Hatimaye, utengano huu, bila kujali kama ni kwa mpito au kwa utaratibu wa kudumu, kwa kiasi fulani au kwa ujumla, utasababisha madhara katika uzima na ustawi wa kiumbehai husika. Hata kifo kinaweza kutokea kwa sababu yauamuzi wetu.

**Tatu**, na kwa kuhitimisha, inafuata kimantiki kwamba, kwa ajili ya kuhami uzima wa kiumbehai anayeitwa binadamu na kukuza ustawi wake, inaonekana kwamba “tunapaswa” kuheshimu kanuni za kibinadamu kuhusu uzima na ustawi wa watu, kama zinavyodhihirishwa na maumbile ya kiumbehai husika.





## Nani anabeba hatma ya Fei?

Na Yusuf **ABOUD**

**S**AKATA la mchezaji wa Yanga, Feisal Salum Abdalla (Fei Toto), bado bichi na linaonekana kumuweka njiapanda.

Hivi sasa bado yeye mwenyewe anahaha. Hajui nani anashikilia hatma yake. Familia yake, kupitia kwa mama yake, imeamua pia kujitokeza na kuomba apate “haki.”

Hata hivyo, sheria za soko zinathibitisha kuwa Fei Toto alikosea njia za kutaka kuondoka Yanga.

Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ya Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) ilitoa uamuzi kwamba mchezaji huyo ni halali wa klabu hiyo kwa mujibu wa mkataba uliopo na waajiri wake, baada ya kubaini kuwa alivunja baadhi ya sheria katika nia yake ya kuondoka kwenda kujiunga na timu nyingine.

Baada ya uamuzi huo, Fei Toto anadaiwa kutamani kukata rufaa kupinga uamuzi huo, ingawa kufanya hivyo kunaonekana kuwa na hasara zaidi kwake kuliko faida anayoitegemea. Tuone baadhi ya hasara hizo.

Endapo mchezaji huyo atapeleka shitaka lake, kwenye Mahakama ya Usuluhishi (CAS) ya Shirikisho la Soka la Kimataifa (FIFA) kuna uwezekano mkubwa wa kushindwa mapema kwani imedhihirika kuwa alighafirika kufikia uamuzi huo.

Kwamba kabla ya kuvunja mkataba, alitakiwa kwanza kupeleka maombi Yanga ya kutaka kuvunja mkataba na kueleza sababu za kufanya hivyo. Fei Toto hakufuata utaratibu huu, yeye alilipa aliyoiita fidia, kisha akaandika barua ya kuvunja mkataba. Hii haikubaliki.

Kwamba muda wa kuvunja mkataba haukuwa sahihi, mkataba hauvunjwi katikati ya msimu, labda kuwe na sababu maalum, lakini siyo za kutokuwa na mahaba na timu, au kupata timu nyingine. Mikataba inayovunjwa kwa kupata timu nyingine, huvunjwa kwa



Fei Toto

makubaliano na lazima timu anayotaka kwenda mchezaji, iombe ruhusa kutoka kwa klabu yake aliyo na mkataba nayo.

Kwamba madai ya Fei ya kuvunja mkabata, hayatokani na Yanga kukiuka makubaliano kwenye mkataba, wala yeye kupata majeraha, wala ubaguzi wa rangi, wala unyanyasaji wowote au mazingira magumu katika utekelezaji wa kazi yake, hivyo, FIFA hawawezi kukubali upuuzi wa kuvunja mkataba kirahisi.

Kwamba Feisal kukimbia mazungumzo na Yanga ni kujichelewesha tu, kwa sababu, kawaida ya FIFA ni kutaka mchezaji acheze ili kulinda kipaji chake, hivyo wakati wanaendelea kushughulikia kesi yake, watamwambia arudi klabuni kwake akacheze, mpaka shauri lake litakapopata uamuzi.

Kwamba Feisal akipeleka kesi FIFA na ikabainika kuna klabu ilimshawishi kuvunja mkataba, uwezekano wa FIFA kuifungia klabu hiyo kusajili misimu miwili mpaka mitatu ni mkubwa na hata Feisal mwenyewe anaweza kufunguwa na FIFA.

**Mwandishi ni mbobexi kwenye uchambuzi wa soka.**

# ONA MLIMA KILIMANJARO



*Sehemu ya juu kabisa ya Mlima Kilimanjaro inavyoonekana kutoka angani. Picha hii imepigwa juzi na John Ulanga akiwa ndani ya ndege kutoka Nairobi, Kenya kurejea Dar es Salaam, Tanzania.*

GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.

